# Kiongozi cha Msaada wa Mzazi kwa Vigezo vya Pamoja vya Msingi vya Jimbo

engage ny
Our Students. Their Moment.

## SANAA ZA LUGHA YA KIINGEREZA NA HISABATI

Mwaka wa2010, Bodi ya watawala wa New York walichagua Common Core State Standards (CCSS) kuhakikisha kwamba watoto wote wanafanikiwa wanapo maliza sekondari. Muongozo huu umebuniwa kukusaidia kuelewa namna kanuni hizi zitakavyo badili mtoto wako, mabadiliko gani ambayo utakayoyaona na nini unaweza kufanya kumsaidia mtoto wako darasani.

### Kwa nini The Common Core State Standards ni Muhimu?

The Common Core State Standards ni muhimu kwa sababu itawasaidia watoto wote – bila ya kujali wao nani – wajifunze ustadi moja. Wanaviumba wazi matumaini ya vile mtoto wako anapaswa kujua na kuweza kufanya kwenye maeneo muhimu: **kusoma, kuandika, kuzungumza** na **kusikiliza lugha na hisabati**. Ukijua haya matumaini, basi unaweza kushirikiana na mwalimu kumsaidia mtoto wako kujiadaa.

## SANAA ZA LUGHA YA KIINGEREZA (ELA)

The Common Core State Standards vinafanya mabadiliko muhimu kwenye viwango vilivyopo sasa. Mabadiliko haya yanaitwa mageuzi. orotha hapo chini inaonyesha nini haya mageuzi hubadilika, nini unaweza kuona katika mkoba ya mtoto wako na nini unaweza kufanya ili kumsaidia. Ikiwa kazi ya mtoto wako haitafakari mageuzi haya, basi zungumuza na mwalimu wake.

| Kipi Kinageuka? | Kipi cha Kukitazamia kwenye Mkoba? | Kipi Unachoweza Kufanya? |
|---|---|---|
| • Sasa mtoto wako atasoma zaidi **zisizo za uongo** kila daraja | • Tazamia mtoto wako kuwa na kazi zaidi za kusoma kulingana na matukio halisi ya maisha, kama vile,maandiko ya habari za maisha ya watu, makala na hadithi za kihistoria. | • Soma vitabu vyenye hadithi zisizo za uongo na watoto wako. Tafuta namna ya kufanya usomaji kuwa jambo la kufurahisha na msisimko. |
| • Kusoma zaidi nakala zisizo za uongo kutamsaidia mtoto wako **kujifunza dunia kupitia kusoma**. | • Tazamia watoto wako kuleta nyumbani vitabu zaidi vyenye ukweli kulingana juu ya ulimwengu. Kwa mfano, mtoto wako wa daraja la kwanza au Chekechea anaweza kusoma kitabu kiitwacho *A Tree is a Plant* cha Clyde Robert Bulla. Kitabu hiki huwawezesha wanafunzi kusoma na kujifunza kuhusu sayansi. | • Juwa ni vitabu vipi visizo za uongo ni kiwango cha daraja sahihi na hakikisha watoto wako wanaweza kuvipata vitabu hivyo. |
| • Watoto wako watasoma **nakala zenye changamoto kwa ukaribu zaidi**, ili waweze kupata maana ya kile wanachosoma na kupata hitimisho lao wenyewe. | • Watoto wako watakuwa na kazi za kusoma na kuandika ambazo zinaweza kuwauliza kusimulia au kuandika kuhusu sehemu muhimu ya hadithi au kitabu. Kwa mfano, mwanao wa daraja la 2 au 3, anaweza kuulizwa kusoma kwa sauti kitabu cha Faith D'Aluisio kisicho cha kubuni kiitwacho *What the World Eats* na kusimulia ukweli kutoka kwenye hadithi hiyo. | • Wape watoto wako maandiko zaidi ya kusoma yenye changamoto. Waonyeshe namna ya kuchimba kwa undani kwenye vipande vigumu |
| • Panapohusika kuandika na kusimulia hadithi, watoto wako **watatumia "ushahidi" uliokusanywa kwenye nakala ili kuunga mkono kile wanachosema.** | • Tazamia kazi za kuandika ambazo zinauliza mtoto wako kuteka juu ya mifano halisi kutoka kwenye maandishi yanayotumika kama ushahidi. Usahidi humaanisha mifano kutoka kwenye kitabu ambacho mtoto wako atatumia kuunga mkono jawabu au hitimisho. Hii ni tofauti kutoka maswali ya maoni ambayo imekuwa ikitumika zamani. | • kuuliza mtoto wako kutoa ushahidi katika majadiliano yakila siku na kutoelewana. |
| • Watoto wako **watajifunza namna ya kuandika kutoka kile wanachosoma.** | • Tazamia kazi za kuandika ambazo zinamuuliza mtoto wako kuunda hoja katika maandishi kwa kutumia ushahidi. Kwa wanafunzi wa daraja la 4 na 5, hii inaweza kumaanisha kusoma na kuandika juu ya *The Kid's Guide to Money,* kitabu isiyo ya uongo ya Steve Otfinoski. | • Mpe moyo kuandika akiwa nyumbani. Andika pamoja naye mukitumia ushahidi na taarifa za undani |
| • Mtoto wako **atakuwa na ongezeko la msamiati wa kitaaluma.** | • Tazamia kazi ambazo zitaeneza msamiati wa watoto wako na kumfundisha kwamba "lugha ni nguvu." | • Mara nyingi wasomee watoto wachanga, wasioanza skuli na watoto |

## HISABATI

Ili kuboresha wanafunzi kujifunza.TheCommon Core State Standards ni tofauti na ile ya zamani. Mabadiliko haya yanaitwa mageuzi. orodha hapo chini inaonyesha nini ni mageuzi, nini unaweza kuona katika mkoba ya mtoto wako na nini unaweza kufanya ili kumsaidia.Tena, ikiwa kazi ya mtoto wako haitafakari mageuzi haya, basi zungumza na mwalimu wake.

| Kipi Kinageuka? | Kipi cha Kukitazamia kwenye Mkoba? | Kipi Unachoweza Kufanya? |
|---|---|---|
| • Mtoto wako **atafanya kazi zaidi kwa undani mada chache**, ambazo zitahakikisha ufahamu kamili (takribani!) | • Tazamia kazi ambazo zinahitaji wanafunzi kuonesha kazi zao na kuelezea namna walivyopata jawabu. | • Juwa dhana gani ni muhimu kwa watoto wako kulingana na kiwango cha daraja yao na tumia muda kufanya kazi katika dhana hizo. |
| • Mtoto wako ataendelea **kujijenga juu ya kujifunza mwaka baada ya mwaka**, kuanzia na msingi imara. | • Tazamia kazi ambazo zinamujenga mtu mwingine. Kwa mfano, wanafunzi watalenga kwenye kujumlisha, kutoa, kuzidisha na kugawa. Mara maeneo haya yamefuzu, watalenga fractions. Kutoka hapo, watajikita kwenye Algebra(hesabu inayotumia herufi dadala ya tarakimu). Pia utaweza kuona maendeleo kwenye mada wanazojifunza. | • Kuwa na ufahamu wa dhana gani ambazo zilimpa tabu mtoto wako mwaka jana na umtegemeze mtoto wako katika maeneo changamoto ili asonge mbele. |
| • Mtoto wako **atatumia muda kufanya mazoezi na kukariri ukweli wa kihisabati** | • Tazamia kazi ambazo zinamuuliza mtoto wako kufuzu kihesabu kama vile kujumlisha makundi hadi ya 20 au majadweli ya kuzidisha. | • Jadiliana na mtoto wako kujua na kukariri ukweli wa msingi wa hisabati. Mtake "fanya hisabati" ambayo inahusiana na maisha ya kila siku. |
| • Watoto wako **watafahamu kwa nini hisabati hufanya kazi na wataulizwa kujadiliana kuhusu na kuthibitisha ufahamu wao.** | • Watoto wako wanaweza kuwa na kazi ambazo zinawauliza kuonesha au kuelezea fikira ya kihisabati – KUSEMA kwa nini wanafikiri jibu lao ni sahihi. | • Jadiliana na watoto wako juu ya kazi zao za nyumbani za hisabati na uwaulize wakufundishe dhana mpya. kufikiri namna ya kuelezea mawazo yao. |
| • Mtoto wako sasa atauliziwa **kutumia hisabati kwenye hali halisi ya maisha** | • Tazamia kazi za hisabati ambazo zinalingana kwenye uhalisia. Kwa mfano, kazi ya nyumbani za wanafunzi wa daraja la 5 linaweza kuwapamoja na kujumlisha fractions kama sehemu ya mapishi au kuamua kiasi gani cha pizza marafiki walikuwa kwa msingi wa frctions. | • Mpe mtoto wako muda kila siku kufanya kazi za hisabati nyumbani. |

## KUZUNGUMZA NA MWALIMU WA MTOTO WAKO

Unapozungumza na mwalimu wa mtoto wako, jaribu kuyafanya mazungumzo hayo yalenge mada yalio muhimu zaidi ambayo yanahusiana na mtoto wako. Hii inamaanisha kumuuliza mwalimu namna mtoto wako anafanya kulingana kwa viwango vya daraja na matarajio.

Pia, omba kuona mfano wa kazi ya mtoto wako. Linganisha mifano ya kazi za mtoto wako na zile zinazopatikana kwenye http://www.engageny.org/resource/new-york-state-common-core-sample-questions. Pia, kuwa huru kuileta mifano hiyo kwa mwalimu wa mtoto wako na kuuliza mwalimu akuelezee namna mifano hiyo inavyotumika darasani.

Habari hii itakuwezesha kufanya marekebisho muhimu nyumbani ambayo yanaweza kumsaidia mtoto wako kupata mafanikio darasani.

***Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea: www.engageny.org ama wasiliana na mwalimu mkuu au msimamizi. kwenye eneo lako.***